**SUMAIT University Journal (SUJ)**
eissn (2953-2698)
Issue No.18, June ,2026

# VIPENGELE VYA UTAMADUNI KATIKA RIWAYA ZA *DESERTION*, *LAST GIFT NA PARADISE* ZA ABDULRAZAK GURNAH

**Mafunda Salum Ali**
*massab463@gmail.com*
*Idara ya Kiswahili na lugha za kigeni*
*Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar*
**Zainab Ali Iddi**
*zeinabiddi@yahoo.com*
*Idara ya Kiswahili na lugha za kigeni*
*Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar*

*Received: October 20225, Accepted: December 2025, published June 2026*
*© SUMAIT University Journal 26*

**Abstract:**

*This article focuses on a study that examines elements of Swahili culture in the novels as Desertion, The Last Gift, and Paradise. The main objective of the article was to determine the extent to which these works embody Swahili culture, given that Abdulrazak Gurnah is a Swahili born and raised in Zanzibar, who has lived abroad for most of his life wrote in English. To what extent, then, do these works reflect Swahili cultural heritage? The study was guided by Diaspora Theory as discussed by various scholars such as [27], as well as other contributors including [34], [31], among others. The article employed a descriptive (qualitative) approach in collecting and analysing data. The document analysis method was used, whereby the researcher carefully read the novels as Desertion, The Last Gift, and Paradise and subsequently extracted relevant data. The findings of this study reveal that there are various elements of Swahili culture in these novels. Among these elements are: Swahili marriage and wedding customs, Swahili occupations, Swahili belief systems, Swahili greetings, funeral and burial practices, and language. Finally, the researcher concludes that there is a need for further investigation into the works of Swahili authors living in the diaspora, in order to understand the extent to which these artists are influenced by the environment in which they were born and currently reside.*

**Keywords:** Novel, Culture, Diaspora, Swahili, Diaspora Life, English.

**Ikisiri**

*Utafiti huu ulichunguza usawiri wa utamaduni wa Mswahili katika riwaya teule za Abdulrazak Gurnah, ambazo ni [9], [11] na [10]. Lengo kuu la utafiti lilikuwa kuchunguza jinsi vipengele vya utamaduni wa Mswahili vinavyosawiriwa katika riwaya hizo. Utafiti huu umetumia Nadharia ya Diaspora iliyoasisiwa na [12], [7] na [5], ambayo iliwezesha kuchunguza namna fasihi ya uhamaji inavyohifadhi au kubadili utambulisho wa kiutamaduni katika mazingira mapya. Mbinu ya kimaelezo ilitumika katika utafiti huu,*

*ambapo data za msingi zilikusanywa kwa kutumia udurusu matini. Riwaya tatu ziliwasilishwa kama sampuli ya maandiko ya Gurnah, huku mbinu ya usampulishaji lengwa ilitumika katika kuchagua riwaya husika. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa vipengele vya utamaduni wa Mswahili kama vile lugha, kazi, chakula, mavazi, maamkizi, msiba na kifo, pamoja na itikadi, ambavyo vimesawiriwa katika riwaya teule. Aidha, utafiti ulibaini kuwa fasihi ya Gurnah ni nyenzo muhimu ya kuhifadhi na kuendeleza utamaduni wa Kiswahili katika muktadha wa uhamaji na mabadiliko ya kihistoria. Kwa jumla, utafiti huu unatoa mchango mpya kwa taaluma ya fasihi na masomo ya utamaduni kwa kuonesha jinsi maandiko ya Gurnah yanavyoweza kutumika kama marejeleo ya utafiti kuhusu utambulisho na urithi wa Waswahili katika mazingira ya sasa ya ughaibuni.*

## 1. UTANGULIZI

Kwa mujibu wa utafiti huu waswahili ni watu wanoishi katika mwambao wa Afrika Mashariki, ambao wana utamaduni wao wanaoufuata katika maisha ya kila siku. [21] anaonesha kuwa utamaduni wa Mswahili unahusu mila, asili, jadi, na desturi za mavazi, vyakula, imani, tabia, na maisha ya jamii kwa jumla. Malezi ya Kiswahili yameelezwa kutilia sana mkazo dhana ya heshima katika mapana yake. Vyuo vya kurani na maulidi na kumbini ni taasisi mbili zilizoelezea makuzi na malezi ya Waswahili. [3] anaeleza kuwa: Utamaduni wa Mswahili umebeba mila na desturi ambazo zimekuwa zikitumika kama sheria na kuwaongoza wanajamii kutenda matendo yanayopaswa kutendeka katika jamii. Utamaduni wa kazi za Waswahili ni pamoja na uvuvi, ukwezi, ukulima, usafiri wa baharini, biashara, ufundi mbalimbali pamoja na uundaji wa vyombo vya bahari na kadhalika [21].

Kwa mnasaba wa maelezo hayo ni dhahiri kuwa tafiti mbalimbali zimekuwa zikionesha utamaduni wa Mswahili ulivyosawiriwa na waandishi wa kazi mbalimbali za fasihi. Miongoni mwa wanafasihi waswahili ambao wameandika kazi za fasihi ikiwemo riwaya ni mwandishi Abdulrazak Gurnah. Mwandishi huyu ameandika riwaya kama vile: *Admiring Silence*, *Desertion*, *By the sea*, *Memory of Departure*, *Pilgrims Way*, *Dottie*, *Last Gift*, *Paradise.* Hata hivyo watafiti hao kwa ufahamu wa mtafiti hakuna mtafiti aliyeangazia kuchunguza jinsi utamaduni wa Mswahili unavyosawiriwa katika riwaya za Abdulrazak Gurnah kama kazi za fasihi. Lililomshawishi zaidi mtafiti kufanya utafiti huo ni kwamba Abdulrazak Gurnah alizaliwa Zanzibar, hivyo ni Mswahili wa Zanzibar kwa kuzaliwa. Utamaduni wa Zanzibar ni utamaduni wa Mswahili. Hivyo kwa mantiki hiyo A.Gurnah ni Mswahili na ameandika riwaya mbalimbali, ambapo inadhaniwa kwamba amezungumzia mambo mengi ya maisha ya Mswahili. Mwandishi anayezungumzia maisha ya Mswahili ni lazima atazungumzia utamaduni wa mtu huyo. Kwa hivyo inatarajiwa kwamba mwandishi amefanya hivyo katika riwaya zake.

Jambo la kujiuliza ni kwamba je, mwandishi huyu ambaye aliondoka Zanzibar na kuhamia ughaibuni – Uingereza kwa muda mrefu (miongo kadhaa) na kuishi kwenye jamii yenye utamaduni tafauti na wa Mswahili, amemudu kuutumia vizuri utamaduni wa Mswahili katika riwaya zake? Mtafiti ameona hapo pana jambo ambalo linahitaji kuchunguzwa kwa njia ya utafiti ili jamii ya Waswahili na watu wengine ulimwenguni kulielewa hilo. Hivyo mtafiti anataka kuchunguza

usawiri wa utamaduni wa Mswahili katika riwaya za Abdulrazak Gurnah Mfano kutoka katika [11], [10] na [9].

### 2. MBINU ZA UKUSANYAJI WA DATA

Ukusanyaji wa data ndio hatua muhimu katika utafiti wa kisayansi. [17] anafafanua dhana ya ukusanyaji wa data kama zoezi la awali katika utafiti ambalo humuwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kumfikisha katika madhumuni yake ya utafiti. Aidha, [17] anasisitiza kuwa hatua ya uwasilishaji na uchambuzi wa data haiwezi kufanyika kabla ya hatua hii ya ukusanyaji wa data. Katika utafiti huu, data zilikusanywa kwa kutumia njia ya udurusu matini.

### 2.1 MBINU YA UDURUSU MATINI

Mbinu ya udurusu matini, mtafiti alidurusu kwa makini riwaya teule za *Desertion, Last Gift na Paradise* kwa makini  huku akidondoa data anazozikusudia. Wakati wa kukusanya data kutoka kwenye maandiko hayo mtafiti alisoma kwa umakini mkubwa neno, kirai na kila sentensi huku akiwa ananukuu data anazozikusudia ambazo zimejibu maswali ya utafiti wake. Data zilikusanynwa na kuchambuliwa kwa njia ya maelezo, kama ambavyo utafiti huu umetumia mkabala wa kitaamuli.

### 3. KIUNZI CHA NADHARIA

Mtafiti anakusudia kuchunguza usawiri wa utamaduni wa Mswahili katika riwaya tatu za Abdulrazak Gurnah. Hivyo basi, utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Dayasfora.Nadharia hii imefafanuliwa na wataalamu mbalimbali duniani kama vile; [27], Baadhi ya wataalamu wengine wanaotoa mchango wao ni [6], [14], [26], [31], [8].

### 3.1 Nadharia ya Dayaspora (Diaspora Theory)

Nadharia ya dayaspora inaangazia jinsi watu wanavyotawanyika kutoka kwa makazi yao ya asili na kuishi katika maeneo mengine, na jinsi wanavyoendeleza utamaduni wao na kujenga utambulisho wa kipekee katika nchi za kigeni.

### 3.2 Mihimili ya Nadharia ya Dayaspora

1. Uundaji na sababu za uhamaji. Inachunguza sababu zinazowafanya watu kuondoka makwao, kama vile migogoro, vita, au nafasi za kiuchumi. Inaangalia pia jinsi uhamaji huu unavyoleta ushawishi katika maisha ya wahamiaji na jamii walizoziacha.
2. Uhifadhi wa utamaduni na utambulisho. Inachunguza jinsi jamii za wahamiaji zinavyohifadhi mila, desturi, na lugha zao huku wakijaribu kuendana na mazingira mapya. Pia inaonesha jinsi utamaduni wa diaspora unavyojibadilisha na kuathiriwa na mazingira ya kigeni.
3. Uhusiano wa kimataifa (Transnationalism). Hii inahusisha jinsi diaspora inavyoungana na nchi zao za asili kupitia shughuli kama kutuma pesa, kuwasiliana, na kushiriki katika siasa. Inachunguza athari za uhusiano huu kwa nchi za asili na nchi za makazi.
4. Mitandao ya kijamii na ujenzi wa jamii. Diaspora mara nyingi huunda mitandao na jamii zinazowasaidia kujisikia nyumbani katika nchi za kigeni. Vilevile inachunguza jinsi mitandao hii inavyofanya kazi na umuhimu wake katika maisha ya wahamiaji.

5. Mchanganyiko na uzoefu wa kuishi pamoja inachunguza jinsi wahamiaji wanavyoshirikiana na jamii za wenyeji na changamoto zinazotokana na kujaribu kuungana na kutambulika katika jamii mpya.
6. Madhara kwa nchi za mwenyeji na nchi za asili. Diaspora anaweza kuwa na athari kubwa kwa nchi wanazokalia na nchi za asili, ikijumuisha mchango katika maendeleo ya kiuchumi, mabadiliko ya kisiasa, na utoaji wa msaada wa kijamii.

Nadharia hii inasaidia kuelewa jinsi diaspora inavyoathiriwa na inavyoathiri mazingira ya kigeni, na jinsi inavyochangia katika kuunda jamii na utamaduni mpya.

Utafiti huu ulitumia nadharia hii kwa sababu ilimsaidia kuchambua malengo yake vizuri. Hususan muhimili wa pili unaosomeka. Uhifadhi wa utamaduni na utambulisho. Inachunguza jinsi jamii za wahamiaji zinavyohifadhi mila, desturi, na lugha zao huku wakijaribu kuendana na mazingira mapya. Muhimili huu ulisaidia kuchambua lengo la utafiti huu la kubainisha ujitokezaji wa vipengele vya utamaduni wa Mswahili katika riwaya teule.

**4. MATOKEO YA UTAFITI**

Baada ya uchunguzi wa kina mtafiti amegundua kuwa pamoja na kuwa A. Gurnah amehamia ughaibuni lakini anaendeleza vyema utamaduni wa mswahili kwa kutunga riwaya zinazoandikwa kwa lugha isiyo kuwa ya Kiswahili yenye kusheheni vipengele vya utamaduni wa mswahili.

Jedweli linaloonesha mchanganuo wa vipengele vya utamaduni

| **Vipengele vya utamaduni vilivyojitokeza katika riwaya teule** | | |
|---|---|---|
| ***Desertion*** | ***The Last Gift*** | ***Paradise*** |
| Kazi | chakula | Kazi |
| Chakula | lugha | Chakula |
| Lugha | maamkizi | Lugha |
| Maamkizi | mazishi | Mavazi, mazishi |
| Itikadi | | Maamkizi , Itikadi |

**4.1 Vipengele vya Utamaduni wa Mswahili katika Riwaya Teule**

Sehemu hii inahusu uchambuzi wa lengo la utafiti ambalo lililenga kuchambua vipengele vya utamaduni wa Mswahili kama vinavyosawiriwa katika riwaya teule za Abdulrazak Gurnah. Fasihi, hususan riwaya, ni nyenzo muhimu ya kuhifadhi na kurithisha historia na utamaduni wa jamii kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kwa mujibu wa [23] na [19] kazi za fasihi huchukua nafasi ya kuhifadhi uhalisia wa maisha ya jamii kupitia masimulizi ya kifasihi yanayowasilisha mila, desturi, na maisha ya kila siku. Katika muktadha huu, riwaya za *Paradise* [9], [11], na [10] zimehifadhi vipengele vya utamaduni wa Mswahili kwa kusawiri maisha ya jamii hiyo kwa kina.

Sehemu hii inajibu swali mahususi la utafiti: "Ni vipi vipengele vya utamaduni wa Mswahili vinavyojitokeza katika riwaya ya *Desertion*, *The Last Gift*, na *Paradise*?" Matokeo ya uchambuzi wa riwaya hizi yanaonesha kuwa vipengele vya kazi, chakula, lugha, mavazi, kifo na mazishi, maamkizi, na itikadi vimesawiriwa katika riwaya hizi. Kwa kuongozwa na Nadharia ya Dayaspora, mjadala huu unachunguza jinsi vipengele hivi vilivyowasilishwa katika kazi ya fasihi ya Gurnah na nafasi yake katika kuhifadhi urithi wa Waswahili, hasa kwa kuzingatia kuwa mwandishi aliandika kazi hizi akiwa nje ya jamii yake ya asili.

#### 4.1.1 Kuonesha kazi za waswahili

Kazi ni sehemu muhimu ya utamaduni wa jamii yoyote, kwani huainisha njia za kujipatia riziki na nafasi ya kijamii ya mtu. Kwa mujibu wa Nadharia ya Dayaspora, fasihi ya wahamiaji mara nyingi hubeba kumbukumbu za maisha ya jamii zao za asili, ikiwemo kazi zao za jadi. Katika riwaya za Gurnah, kazi za Waswahili zimesawiriwa kwa kina, zikionesha jinsi utamaduni huu unavyoendelea hata katika mazingira ya mabadiliko ya kihistoria.

Katika [9], mwandishi anasawiri biashara kama sehemu kuu ya maisha ya Waswahili. Ami Aziz, mmoja wa wahusika wakuu, ni mfanyabiashara mashuhuri anayeheshimika kwa nafasi yake ya kiuchumi. Nukuu ifuatayo inaonesha heshima aliyopewa kutokana na kazi yake:

> *"His father said they brought honour on them because he was a rich and great merchant" (uk. 3).*
>
> *(Baba yake alisema kwamba ujio wake ulileta heshima kwao kwani alikuwa mfanyabiashara mkubwa. TY)*

Katika data hiyo tunaona kuwa biashara si tu njia ya kupata riziki bali pia ni kipengele cha heshima na hadhi katika jamii ya Waswahili. Hoja hii inalingana na hoja ya [20] kwamba biashara imekuwa kiini cha ustawi wa jamii za pwani ya Afrika Mashariki tangu enzi za biashara ya Bahari ya Hindi. Pia, riwaya inaonesha kazi za jadi za Waswahili, kama vile ufumaji wa kofia za hariri:

> *"An old man who sat on a stool on the pavement at the storefront, embroidering caps with silk thread" (uk. 5).*
>
> (Na mzee mmoja aliyekaa kwenye kigoda kilichokuwa kwenye kibaraza mbele ya duka huku akifuma kofia kwa uzi wa hariri… TY)

Data hiyo inathibitisha kuwa kazi za mikono kama ufumaji zilikuwa sehemu ya utamaduni wa kiuchumi wa Waswahili, jambo linaloendana na dhana ya *"economic memory"* inayozungumziwa na [7] katika nadharia yake ya Dayaspora, ambapo wahamiaji huhifadhi kumbukumbu za uchumi wa jamii zao kupitia fasihi na sanaa.

Katika [11], kazi za jadi zinaendelea kusawiriwa, ambapo wahusika wanahusishwa na kazi kama ushonaji wa mikoba, upakaji rangi nyumba, na uuzaji wa vyakula vya asili:

> *"Kipara had been a basket weaver and Jumanne had been a house painter… Aunt Mariyam started a business frying samosa and bajia which she made to order for functions" (uk. 80).*

(Kipara alikuwa mshona mikoba na Jumanne alikuwa mpakaji rangi nyumba… Shangazi Maryam alianza biashara ya kuchoma sambusa na bajia kwa oda maalumu. TY)

Data hiyo inadhihirisha kuwa kazi ni sehemu ya utamaduni wa Waswahili ambapo Waswahili wanafanya kazi za jadi kama vile kushona mikoba, kupaka rangi nyumba, na kufanya biashara ndogondogo. Aidha, katika [10], mwandishi anaonesha kuwa Waswahili walihusika pia na kazi za viwandani na utafsiri wa mashairi, akieleza:

*"She told him her name too and said that she worked in a factory" (uk. 16).*

(Alimwambia jina lake pia na alisema kuwa anafanya kazi katika kiwanda. TY)

Katika data hiyo pia tunabaini kuwa Waswahili si tu wanafanya kazi za jadi na biashara ndogo ndogo majumbani bali pia wanafanya kazi katika viwanda. Kwa hivyo, Gurnah anatumia riwaya zake kuhifadhi kumbukumbu za kazi za jadi za Waswahili, huku pia akionyesha jinsi jamii hii ilivyobadilika kutokana na uhamaji na athari za ukoloni.

#### 4.1.2 kuonesha chakula cha waswahili

Chakula ni kipengele muhimu cha utamaduni wa jamii yoyote, kwani huwakilisha utambulisho wao wa kitamaduni na historia yao. Kwa mujibu wa Nadharia ya Dayaspora, chakula mara nyingi hubeba maana zaidi ya lishe, kwani kinawakilisha mizizi ya jamii na huweza kuwa sehemu ya mawasiliano ya kitamaduni kwa wahamiaji walioko ughaibuni [12].

Katika [9], Gurnah anasisitiza ulaji wa mashelisheli kama sehemu ya utamaduni wa Waswahili:

*"Not that he thought there was anything wrong with breadfruit. They used to eat it at home cooked in coconut sauce and accompanied with fried sardines" (uk. 64).*

(Sio kwamba yeye alihisi kuna shida yoyote katika shelisheli. Walikuwa wanayala nyumbani yakiwa yamepikwa kwa nazi na dagaa waliokaangwa. TY)

Data hiyo inaonesha jinsi vyakula vya baharini na matumizi ya nazi yalivyokuwa sehemu muhimu ya mapishi ya Waswahili, jambo linalothibitishwa na [1] kwamba utamaduni wa Kiswahili umeathiriwa sana na matumizi ya nazi na vyakula vya pwani. Katika [11], mwandishi anasisitiza umuhimu wa kahawa kwa Waswahili:

*"He went to sit at the café with his friend until the siren went for sunset when they all shared their first cup of coffee of the day before going to the mosque" (uk. 179).*

(Alikwenda kukaa katika mkahawa pamoja na marafiki zake mpaka king'ora cha jioni na wote walipata kikombe cha kahawa kabla ya kwenda msikitini. TY)

Vivyo hivyo, katika [10], mwandishi anaonesha ulaji wa halwa na mandazi kama sehemu ya kifungua kinywa cha Waswahili:

*"They had eggs and mandazi for breakfast" (uk. 138).*

(Walitumia mayai na mandazi kwa kifungua kinywa chao. TY)

Kupitia data hiyo, tunaona mwandishi akibainisha kuwa mayai na maandazi kama sehemu ya kifungua kinywa katika jamii ya Waswahili.Kwani waswahili hutumia vitu vyao vya asili katika ufunguaji wa kinywa.

#### 4.1.3 kuonesha lugha ya Kiswahili

Kwa mujibu wa [33], lugha ni mfumo wa sauti za nasibu zinazotumiwa na watu wa jamii moja wenye utamaduni unaofanana ili kuwasiliana. Lugha ni nyenzo muhimu ya kuhifadhi na kuendeleza utambulisho wa jamii, huku ikitumiwa kama chombo cha kuimarisha mshikamano, kurithisha mila na desturi, na kuonesha thamani ya utamaduni wa jamii husika [13; 16]. Katika muktadha wa fasihi ya Dayaspora, lugha mara nyingi hujitokeza kama kiashiria cha uhusiano kati ya wahamiaji na jamii yao ya asili. Nadharia ya Dayaspora, kama inavyoelezwa na [7] na [5], inasisitiza kuwa lugha ni mojawapo ya vipengele ambavyo wahamiaji huendelea kuhifadhi, hata wanapokumbwa na mazingira mapya yanayowalazimu kutumia lugha tofauti.

Katika riwaya zake, Abdulrazak Gurnah anaonesha jinsi lugha ya Kiswahili inavyoendelea kubeba thamani ya kiutamaduni kwa jamii ya Waswahili, licha ya mwandishi kuandika kwa Kiingereza. Uchanganyaji wa Kiswahili katika maandishi yake unaonesha athari za lugha yake mama, akibainisha kuwa bado ana uhusiano wa karibu na utamaduni wake. Mfano katika [9], mwandishi anatumia maneno ya Kiswahili katika mazungumzo ya wahusika, jambo linalodhihirisha kuwa lugha inatumika kama nyenzo ya kudumisha utambulisho wa jamii ya Waswahili:

> *"The vibarua who were their parents came from all over, from the Usambara highlands north of Kawa."* (uk. 7)
>
> (Vibarua wote ambao ni wazazi wao walitoka sehemu mbalimbali, kutoka nyanda za juu za milima ya Usambara Kaskazini mwa Kawa. TY)

Vilevile, Gurnah anatumia Kiswahili kuonesha dhana za kijamii zinazohusiana na imani na itikadi za Waswahili:

> *"This is not your business and you must not ask useless questions. You will bring … kisirani… bad luck. You want to bring evil on us."* (uk. 49)
>
> (Hii sio kazi yako na usiulize maswali yasiyo na maana. Utaleta... kisirani... na mkosi. Unataka kutuletea uovu. TY)

Data hiyo inaonesha kuwa Gurnah anaendelea kuhifadhi baadhi ya dhana za Kiswahili ambazo haziwezi kufasiriwa kwa ufanisi katika lugha nyingine, jambo linaloendana na hoja ya [20] kuwa lugha ni chombo cha kiutambulisho kinachobeba maana ya kipekee kwa jamii fulani.

Katika [11], matumizi ya Kiswahili yanaonekana kupitia misemo na majina ya matukio ya kidini:

> "She stayed from mfungo mosi until mfungo mosi, She spent Muharram with them, Maulid Nabii, Miraji, Ramadhani, Sikukuu ndogo na Sikukuu Kubwa." (uk. 57)

(Alikaa kutoka Mfungo Mosi hadi Mfungo Mosi. Alisherehekea Muharram pamoja nao, Maulid ya Nabii, Miraji, Ramadhani, sikukuu ndogo na sikukuu kubwa. TY)

Data hiyo inaonyesha jinsi lugha ya Kiswahili inavyotumika kuwakilisha muktadha wa kidini wa Waswahili, jambo ambalo linaendana na hoja za [26] kuhusu nafasi ya lugha katika kuhifadhi historia na itikadi za jamii. Katika [10], mwandishi anaendelea kutumia Kiswahili ili kutoa utambulisho wa jamii ya Waswahili katika simulizi zake:

"The man from the Government was tall and thin, and dressed in a kanzu and kofia." (uk. 59)

(Mwanaume kutoka Serikalini alikuwa mrefu na mwembamba, na amevaa kanzu na kofia. TY)

Katika data hiyo, kanzu na kofia ni mavazi yenye asili ya Kiswahili, na matumizi ya maneno haya ndani ya Kiingereza yanaonesha kuwa mwandishi anadumisha urithi wa jamii yake kupitia lugha. Kwa hivyo, Gurnah anatumia lugha kama daraja la kuunganisha jamii ya Waswahili na historia yao, jambo linaloendana na maelezo ya [5] kuhusu Dayaspora kuwa sio tu kuhama kimwili, bali pia ni mchakato wa kuhama na kuhifadhi utambulisho wa kijamii na kiutamaduni kupitia lugha.

#### 4.1.4 kuonesha mavazi ya mswahili

Mavazi ni sehemu muhimu ya utambulisho wa kitamaduni wa jamii, yanayoonesha nafasi za kijamii, heshima, na mila za watu husika. Kwa mujibu wa [21] na [15], mavazi yanaweza kuonyesha mfumo wa maisha wa jamii fulani na mara nyingi hutumika kama kiashiria cha utambulisho wa kijinsia, kidini, na hata kijamii.

Katika [9], Gurnah anatumia mavazi kuonesha namna Waswahili wanavyothamini heshima na hadhi kupitia mavazi yao. Mfano katika dondoo ifuatayo:

"Her frilled white blouse was buttoned up at the neck and wrists, and her long skirt brushed her shoes." (uk. 1)

(Blausi yake iliyokuwa na marinda ilifungwa kwa vifungo vilivyofika shingoni na vingine kwenye mikono, gauni yake ndefu ilifagia viatu vyake. TY)

Data hiyo inaonesha jinsi mavazi ya wanawake wa Kiswahili yanavyosisitiza heshima na stara, jambo hilo linatujuilisha kwamba mavazi katika jamii za Kiislamu ya pwani ya Afrika Mashariki yanabeba maana zaidi ya kifuniko cha mwili pia ni alama ya hadhi na utambulisho wa kijamii.

Vilevile, mwandishi anaonesha mavazi ya kiheshima kupitia matumizi ya buibui katika jamii ya Waswahili:

*"Women visitors came, draped from head to toe in black buibui..."* (uk. 36)

(Wageni wa kike walikuja wakiwa wamejifunika buibui nyeusi kutoka kichwani hadi nyayoni. TY)

Katika [11], Gurnah anaendelea kusisitiza uvaaji wa mavazi ya kitamaduni kwa wanawake wa Kiswahili:

> *"She wore a buibui in the street, as all women were expected to do. But her face was uncovered*." (uk. 175)
>
> (Alivaa buibui mtaani, kama wanawake wengine wanavyotarajiwa kufanya. Lakini uso wake ulikuwa wazi. TY)

Katika data hiyo tunabaini kuwa katika jamii ya Waswahili, mavazi haya yanaonyesha heshima na matarajio ya kijamii kwa wanawake. [30] anaeleza kuwa mavazi yanaweza kuwa njia ya kuelezea mfumo wa kijamii, ambapo jamii huweka kanuni kuhusu mavazi kulingana na maadili na heshima inavyopaswa kudhihirishwa.

Aidha, kwa upande wa wanaume, mwandishi anaonyesha kuwa vazi la kanzu ni sehemu ya utambulisho wa mwanaume Mswahili:

> *"That evening at sunset he put on a kanzu and went to the mosque."* (uk. 175)
>
> (Jioni hiyo, alivalia kanzu na kuelekea msikitini. TY)

Kutokana na data hiyo ni dhahiri kuwa Gurnah amesawiri mavazi ya Kiswahili kama kipengele cha kiutamaduni kinachobeba maana ya heshima, utambulisho wa kijinsia, na nafasi ya kijamii. Hii inaendana na Nadharia ya Dayaspora, ambayo inasisitiza kuwa wahamiaji huendelea kuhifadhi vipengele vya mavazi yao kama sehemu ya utambulisho wao wa asili, hata wanapokuwa katika mazingira mapya.

#### 4.1.5 Kuonesha kifo na Mazishi ya waswahili

Kifo ni sehemu isiyoweza kuepukika katika mzunguko wa maisha ya binadamu, na mara nyingi huleta huzuni na upweke kwa jamii inayokumbwa na msiba. Katika jamii ya Waswahili, kifo si tu tukio la kutenganisha mpendwa na jamii kimwili, bali pia huaminika kuwa kuna uwezekano wa kuendelea kuwasiliana na marehemu kupitia mizimu na ndoto [29; 25]. Mtazamo huu wa kifo unaendana na dhana ya Nadharia ya Dayaspora, inayobainisha kuwa jamii za wahamiaji huendelea kuhifadhi mila na itikadi zao za asili, hata wanapokumbwa na mazingira mapya ya kijamii na kiutamaduni [5; 7].

Katika utamaduni wa Waswahili, mazishi ni tukio la kijamii linalohusisha mshikamano wa jamii nzima. Wanafamilia, majirani, na marafiki huungana pamoja kwa ajili ya kumwandalia marehemu mazishi, ambapo wanaume huenda makaburini kwa ajili ya maziko, huku wanawake wakibaki nyumbani kwa ajili ya dua na visomo vya Qur'an. Hili limeelezwa vyema katika [9]:

> *"The wails of the villagers rose inconsolably as the pit was filled in."* (uk. 129)
>
> (Sauti za waombolezaji za wanavijiji, sauti ambazo hazikuweza kutulizika zilipanda wakati shimo lilipokuwa linafunikwa. TY).

Data hiyo inaonesha mshikamano wa kijamii katika maombolezo, ambapo msiba unachukuliwa kama jukumu la jamii nzima badala ya familia pekee. Hii inaendana na maoni ya [22],

anayebainisha kuwa jamii za Kiafrika huona msiba kama tukio linalogusa jamii nzima, ambapo mshikamano huimarishwa kupitia shughuli za mazishi na ibada za kuomboleza.

Aidha, jamii ya Waswahili huamini kuwa baadhi ya vifo husababishwa na husuda na chuki kutoka kwa watu wengine. Husuda huonekana kama nguvu hasi inayoweza kusababisha maangamizi kwa wale waliobarikiwa na neema fulani [20]. Gurnah anazungumzia imani hii katika *Paradise*:

> *"He had lost his wife and infant son only a few months before, through illness and other people's envy. This infant son was the only one of his children who had survived more than a few weeks. All the others had lived long enough to be named, and her husband remembered every one."* (uk. 221)
>
> (Huyo bwana alikuwa amefiwa na mkewe na mtoto wake mchanga wa kiume miezi michache tu iliyopita, hilo lilitokana na maradhi na husuda za watu wengine... TY)

Data hiyo inaonesha imani ya jamii kwamba husuda inaweza kuwa chanzo cha matatizo, ikiwa ni sehemu ya mfumo wa kiimani unaoathiri namna watu wanavyoelewa na kukabiliana na majanga kama kifo. [32] anathibitisha kuwa imani kama hizi ni sehemu ya itikadi zinazotawala jamii za Kiafrika, ambapo matatizo makubwa hupewa tafsiri ya kiroho au kijadi.

Kwa hivyo, Gurnah anatumia *Paradise* kuonyesha jinsi dhana ya kifo katika jamii ya Waswahili inavyofungamana na mshikamano wa kijamii na imani za jadi, jambo linaloonyesha kwamba hata akiwa ughaibuni, mwandishi ameendelea kuhifadhi utamaduni wa jamii yake kupitia fasihi.

#### 4.1.6 Kuonesha maamkizi ya waswahili

Maamkizi ni sehemu muhimu ya utamaduni wa Kiswahili, yanayofanya kazi mbalimbali za kijamii. Kwa mujibu wa [28], (4) na (35), maamkizi yanaweza kuwa njia ya kuonesha heshima, kudumisha uhusiano mzuri, au kutambulisha nafasi ya mtu katika jamii. Katika jamii ya Waswahili, salamu ni sehemu ya kila siku ya maisha, na mara nyingi huambatana na maneno ya heshima na staha.

Katika riwaya za Gurnah, matumizi ya maamkizi ya Kiswahili yanaonesha jinsi lugha inavyotumika kama sehemu ya utambulisho wa jamii, hasa kwa watu walio nje ya jamii yao ya asili. Kwa mujibu wa Nadharia ya Dayaspora, kama inavyoelezwa na [7] na [5], wahamiaji na watu waliotawanyika kutoka jamii zao huelekea kuhifadhi vipengele vya utamaduni wao wa asili, hasa kupitia lugha, mila, na desturi. Katika muktadha wa fasihi ya Gurnah, maamkizi ya Kiswahili yanahifadhi urithi wa Waswahili, yakidhihirisha mshikamano wa kijamii unaoendelea hata katika mazingira ya ukoloni na uhamisho. Kutoka [11]:

> *"Hujambo, mama?" he asked, smiling politely. "Sijambo," she answered, then asked, "Na wewe, hujambo?" (Uk. 32)*
>
> ("Hujambo, mama?" aliuliza, akitabasamu kwa heshima. "Sijambo," alijibu, kisha akauliza, "Na wewe, hujambo?" *TY*)

Katika data hapo juu, tunaona jinsi maamkizi yanavyotumika kuimarisha uhusiano wa kijamii na kudumisha mshikamano. Kwa mujibu wa [28] na [4], maamkizi si tu njia ya mawasiliano, bali pia yanawakilisha mahusiano ya kijamii na heshima kati ya wahusika. Katika jamii za Dayaspora,

maamkizi kama haya ni njia ya kudumisha utambulisho wa tamaduni za asili, jambo ambalo linaendana na hoja ya [12] kwamba wahamiaji huendeleza vipengele vya utambulisho wao wa awali kwa kupitia lugha na mila, hata wanapokuwa katika mazingira ya kigeni.

Aidha, maamkizi Kama kipengele cha utamaduni wa Mswahili kinabainika kutoka Riwaya [10] kama ifuatavyo:

> "*Shikamoo, baba," he said softly. "Marahaba, my son," the old man responded warmly* (Uk. 45)
>
> ("Shikamoo, baba," alisema kwa upole. "Marahaba, mwanangu," mzee alijibu kwa uchangamfu. *TY*)

Data hiyo inaonesha matumizi ya salamu ya heshima ya Kiswahili, ambapo vijana huwasalimu wakubwa kwa kusema "Shikamoo", na wakubwa hujibu kwa **"**Marahaba". Kwa mujibu wa Othman [35], aina hii ya maamkizi inawakilisha heshima kwa wazee na nafasi yao katika jamii. Katika Nadharia ya Dayaspora, hii inaonesha kuwa hata baada ya mabadiliko ya kijamii yanayokuja na uhamaji, watu bado huendelea kuhifadhi desturi zao kwa kupitia lugha na mazoea ya kijamii. [20] anabainisha kuwa maamkizi yanaweza kuwa njia mojawapo ya kudumisha utamaduni wa asili hata katika mazingira ya ugenini.

Pia, kipengele cha utamaduni wa Mswahili cha maamkizi katika riwaya teule za Gurdnah kimejitokeza kutoka Riwaya [9], mwandishi anathibitisha:

> "Salaam aleikum," he said respectfully, bowing his head slightly. The man nodded and replied, "Wa aleikum salaam." (Uk. 10)
>
> ("Assalamu alaikum," alisema kwa heshima, huku akiinamisha kichwa chake kidogo. Mwanaume alitikisa kichwa na kujibu, "Wa alaikum salam." *TY*)

Data hiyo inaonesha matumizi ya salamu ya Kiislamu ambayo ni sehemu muhimu ya maamkizi katika jamii ya Waswahili. Katika Nadharia ya Dayaspora, hii inaonyesha jinsi dini na lugha huchangia katika uundaji wa utambulisho wa jamii za uhamishoni. Kwa mujibu wa [24], lugha ni chombo cha utambulisho wa jamii, na kwa kutumia Kiswahili katika salamu, Gurnah anadumisha uhalisia wa mawasiliano ya Waswahili, licha ya kuandika kwa Kiingereza.

Kwa hivyo, maamkizi katika riwaya za Gurnah yanaonesha jinsi utamaduni wa Kiswahili umeendelea kuhifadhiwa kupitia lugha, hata kwa watu walioko nje ya jamii yao ya asili. Kutumia Kiswahili katika salamu kunaonyesha kuwa lugha ni sehemu muhimu ya utambulisho wa jamii, na kwa mujibu wa Nadharia ya Dayaspora, ni kiungo kinachowaunganisha wahamiaji na historia yao. Katika muktadha wa fasihi ya Gurnah, maamkizi ni zaidi ya maneno ya kila siku—yanawakilisha urithi wa tamaduni, heshima, na mshikamano wa jamii ya Waswahili.

Katika riwaya za Gurnah, wahusika wake hutumia Kiswahili katika maamkizi, jambo linaloonesha kuwa lugha ya Kiswahili si tu chombo cha mawasiliano bali pia ni njia ya kudumisha utamaduni wa jamii. Hili linathibitisha maoni ya [24] kwamba lugha ni chombo cha utambulisho wa jamii, na kupitia matumizi ya Kiswahili, Gurnah anadumisha uhalisia wa mawasiliano ya Waswahili.

#### 4.1.7 Kuonesha itikadi za waswahili

Itikadi ni mfumo wa imani unaoathiri mtazamo wa watu kuhusu maisha na jamii yao kwa ujumla. Kwa mujibu [2] na [18], itikadi inaweza kuwa ya kisiasa, kidini, kiuchumi, au kijamii, na mara nyingi huathiri namna jamii inavyotafsiri matukio yake ya kila siku. Katika muktadha wa *Paradise*, *Desertion*, na *The Last Gift*, Gurnah anasawiri itikadi za Kiswahili zinazohusiana na tiba za jadi, matambiko, na imani kuhusu nguvu zisizoonekana.

Katika [9], mwandishi anaeleza imani ya tiba za jadi na wanga wa Kiswahili:

> *"But she's very ugly. She has a sickness. For many years doctors have come, learned hakim with long grey beards have read prayers for her, and mganga from over the hills have brought medicine, but it's no good..."* (uk. 38)
>
> (Lakini Bibie ni mbovu mno. Ana maradhi kwa miaka mingi. Madaktari walikuwa wanakuja, mashekhe werevu wenye ndevu ndefu zilizojaa mvi wamemsomea dua na waganga kutoka juu ya milima wameleta dawa lakini haikufaa kitu... TY)

Katika data hiyo, tunaona jinsi tiba za jadi na mashekhe wanaosoma dua walivyo sehemu ya itikadi ya matibabu ya Waswahili. Kwa mujibu wa [32], jamii nyingi za Kiafrika zinaaminika kuwa magonjwa makubwa yanaweza kuwa na chanzo cha kisiri au kishetani, na tiba za jadi zinatumika pamoja na zile za kisasa ili kuhakikisha uponyaji wa mgonjwa.

Katika [11], mwandishi anazungumzia imani za matambiko ya kibiashara:

> *"The travellers waited outside the town as was their custom, until permission was granted for entry. A shrine stood nearby, surrounded by snakes and pythons and wild animals. Only if the spirit allowed it could a person reach the shrine safely and leave in peace."* (uk. 136)
>
> (Wasafiri walingoja nje ya mji kama ilivyokuwa desturi yao, hadi hapo ruksa ilipotolewa. Tambiko lilikuwa mbele yao na hilo lilizungukwa na nyoka na chatu na wanyama pori... TY)

Data hiyo inaonesha kuwa Waswahili waliamini kuwa misafara yao ya kibiashara ingeweza kuwa na baraka au mkosi, kulingana na namna walivyoheshimu mila za tambiko. [32] anathibitisha kuwa matambiko ni sehemu muhimu ya jamii nyingi za Kiafrika, ambapo shughuli za kiuchumi na kijamii mara nyingi huanza kwa kufanya tambiko ili kuzuia mkosi au kupata baraka.

## 5. HITIMISHO

Matokeo ya utafiti anaonesha kuwa licha ya mwandishi huyu kuishi nje ya Afrika, bado anaendelea kuhifadhi na kuwasilisha itikadi za jamii ya Waswahili. Fasihi yake inabeba vipengele vya utamaduni wa Kiswahili, ikiwa ni sehemu ya urithi wa Dayaspora unaoendelea kudumishwa katika maandiko yake. Hivyo, Gurnah amesawiri vipengele vya kifo na mazishi, maamkizi, na itikadi kama sehemu ya utamaduni wa Kiswahili unaoendelea kuhifadhiwa na jamii yake ya asili, licha ya mabadiliko ya kihistoria na kiutamaduni.

**MAREJEO**


[1] Allen, J. W. (1971). *Swahili culture and the western Indian Ocean*. Indiana University Press

[2] Ardono, T. (1950). *The authoritarian personality,* New York: Haper.

[3] Bakari, M. (2009). *Swahili culture and identity in East Africa*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota.

[4] Brown, P. (1980). "How and why women are more polite. Some evidence from a Ma-yan community". In McConell-Ginet et al. (eds): Women and language.

[5] Clifford, J. (1994). Diasporas. Cultural Anthropology, 9(3), 302–338. https://doi.org/10.1525/can.1994.9.3.02a00040

[6] Cohen, R. (1997). *Global Diasporas*: *An Introduction. Seattle*: University of Washington Press.

[7] Gilroy, P. (1993). *The Black Atlantic: Modernity and double consciousness.* Harvard University Press.

[8] Giri, B. P. (2007). *Dayaspora and identity: A postcolonial perspective*. Dayaspora Studies, 1(1), 61–78.

[9] Gurnah, A. (1994).*Paradise*. Bloomsbury Publishing. plc.

[10] Gurnah, A. (2021). *Last Gift*. Bloomsbury Publishing. Plc.

[11] Gurnah, A.(2005). *Desertion*. Bloomsbury Publishing.plc.

[12] Hall, E. T. (1990). *Understanding Cultural Differences*: German French Americans. Intercultural Press, Broston.

[13] Hymes, D. (2007). *Foundations in sociolinguistics: An ethnographic approach*. Routledge.

[14] Jain, J. (2006). *Th* Raina, M. L. (2007). "Home, Homelessness and the Artifice of Memory" Contemporary Diasporic Literature: Writing History, Culture, Self. Ed. Manjit Inder Singh. Pencraft *Journa l of Postcolonial Studies*, 12(3), 241–256.

[15] Khamis, S. A. (2007). *Uandishi wa Fasihi Simulizi na Utamaduni wa Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

[16] King'ei, K. (2010).*Misingi ya isimu jamii.* Taasisi ya taaluma za Kiswahili: Chuo kikuu cha

[17] Kothari, C. R. (2014). *Research methodology; method and technigues.* (3rd ed). NewAge International publishing limited. literature and society. 111-136.

[18] Lowenstein, K. (1953). *Political Power and the Governmental Process*. University of Chicago Press.

[19] Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili, historia na misingi ya uchambuzi.* Sitima Printer and stations L.td.

[20] Mazrui, A. A. (2005). The re-invention of Africa: Edward Said, V. Y. Mudimbe, and beyond. Research in African Literatures, 36(3), 68–82.

[21] Mbaabu. I. (Mhar.) (1985). *Utamaduni wa Waswahili*. Nairobi Kenya Publishing & Book Marketing co. ltd.

[22] Mbiti, J. S. (1969). *African religious and Philosophy*. Johannesburg: Heineman.

[23] Mulokozi, M. (1985). *Fasihi na Utamaduni wa Kiswahili*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing

House.
[24] Ngugi, (1986). *Decolonising the mind*: the politicts of language in Africa Literature
[25] Nyonje, R. (2016). *Cultural Perspectives on Death and Mourning Rituals among Swahili people*. Journal of African Traditions, 5(1), 76-92.
[26] Raina, M. L. (2007). *Home, Homelessness and the Artifice of Memory. Contemporary Diasporic Literature:* Writing History, Culture, Self. Ed. Manjit Inder Singh. Pencraft.
[27] Safran, W. (1991). Diasfora *: Journal of transnational studies*. Volume 1, number 1, University of Toronto
[28] Schegloff, E. A. (1968). *Sequencing in conversational openings*. American Anthropologist, 70(6), 1075–1095.
[29] Sengo, T. S. Y. (1992). Utamaduni wa watu wa wilaya ya kusini Unguja. Haikuchapwa.
[30] Simmel, G. (1967). Fashion. *American Journal of Sociology*, 62541-558.
[31] Steiner, G. (1968).Extra Territorial: Papers on Language and Literature.
[32] Swantz, M. L. (1970). *The role of rituals in traditional healing practices among the Swahili*. Dar es Salaam: Tanzania University Press.
[33] TUKI. (1990). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Oxford University Press.
[34] Van H. (2014), *Diaspora Formation*. Migration: A Compass Anthology. Oxford.
[35] Yahya-Othman, S. (1995). *Maamkizi na lugha ya heshima katika Kiswahili*. Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.